Mheshimiwa Mwenyekiti,
Timu ya Menejimenti,
Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa.

TAARIFA YA ZOEZI LA UPIGAJI CHAPA NG'OMBE AWAMU YA PILI HADI KUFIKIA FEBRUARI 28, 2017

1.0 UTANGULIZI

Utekelezaji wa awamu ya pili wa zoezi la usajili na utambuzi wa mifugo na upigaji chapa ng'ombe unazingatia ***Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 ibara ya 3.10*** na ***Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji namba 12 ya mwaka 2010 na kanuni zake za mwaka 2011*** ambazo zinatoa mwongozo wa namna ya kutambua na kusajili wafugaji na Kupiga chapa mifugo yao. Wilaya ya Kilosa kupitia awamu ya kwanza ya zoezi la utambuzi na usajili mifugo imesajili wafugaji 6334 wenye Ng'ombe 176031, mbuzi 122948, kondoo 23436 na Punda 2,258. Jumla ya ng'ombe 60,207 wamepigwa chapa sawa na asilimia 34 ya ng'ombe waliosajiliwa na asilimia 17.2 ya ng'ombe 350,000 wanaokadiriwa kuwepo Wilayani Kilosa. Umuhimu wa zoezi la chapa:-

- Kupunguza au kudhibiti migogoro ya ardhi,
- Kudhibiti wizi wa mifugo
- Kupanga matumizi endelevu ya rasilimali ardhi, maji na malisho.
- Kupanga bajeti ya ujenzi wa malambo, majosho na minada ya mifugo kulingana na idadi ya mifugo.
- Kujua mahitaji ya dawa, josho na chanjo ili kutenga bajeti.
- Baadhi ya wafugaji kuwezeshwa kumiliki maeneo ya ranchi za Taifa (NARCO)

Baadhi ya Changamoto zilizojitokeza awamu ya kwanza ya zoezi la chapa ni Wafugaji hasa wa jamii ya Kimasai kugomea zoezi la chapa na hali ya ukame iliyojitokeza kwa kipindi cha kuanzia mwezi Septemba - Desemba 2016 ni sababu mojawapo zilizochangia kupunguza ufanisi katika zoezi hili la chapa. Ambapo baadhi ya wafugaji waligoma kusajili mifugo yao na Mifugo mingi kuhamishwa kutoka katika maeneo iliposajiliwa kwenda kutafuta maji na malisho.

2.0 AWAMU YA PILI YA ZOEZI LA UPIGAJI CHAPA

Idara inaendelea na utekelezaji wa awamu ya pili kuanzia tarehe 01/02/2017 hadi tarehe 31/03/2017. Katika awamu hii idara ina lengo kupiga chapa hadi kufikia asilimia 80 ya ng'ombe wote waliosajiliwa.

2.1 Shughuli zilizofanyika hadi sasa

- Kutoa elimu juu ya umuhimu wa zoezi la chapa kwa wafugaji katika kata za Parakuyo, Rudewa na Madoto kupitia mkutano wa hadhara wa Mkuu wa Wilaya na wafugaji uliofanyika Parakuyo tarehe 11/02/2017.

- Kutoa maelekezo kwa maafisa watendaji Kata/vijiji, Maafisa Tarafa na Maafisa Ugani mifugo juu ya kuanza kwa awamu ya pili ya zoezi la kupiga chapa mifugo.

- Maandalizi ya Vibanio vya chapa yamekamilika kati vijiji vya Parakuyo na Mkata station.

- Zoezi la upigaji chapa limeanza katika kijiji cha Parakuyo ambapo jumla ya ng'ombe 241 zimeshapigwa chapa. **(Tizama Kiambatanisho B)**

2.2 Changamoto

Katika kutekeleza awamu ya pili ya zoezi la upigaji chapa changamoto zifuatazo zimejitokeza na kupelekea kusua sua kwa zoezi hili:-

- Mifugo mingi bado haijarudi katika vijiji ilikosajiliwa baada ya wafugaji kuhamisha kwenda kutafuta maji na malisho kutokanana na ukame mwishoni mwa mwaka 2016 na kuchelewa kuanza kwa msimu wa mvua za masika mwaka huu.
- Baadhi ya maeneo kutofikika kwa urahisi kwenda kupiga chapa kutokana Hali ya Mvua za masika zilizoanza kunyesha katikati ya mwezi Februari, 2017 hususani maeneo ya Ngaite, Twatwatwa, Kiduhi, Mabwegere.
- Hali ya unyevunyevu kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha inahatarisha kutokea kwa vidonda kwenye ngozi ya ng'ombe baada ya kupigwa chapa hivyo kupunguza ufanisi
- Idara kutokuwa na fedha za usimamizi wa utekelezaji wa zoezi la utambuzi na usajili hivyo zoezi la chapa kukosa usimamizi wa wataalamu kutoka ngazi ya Wilayani.

- Upungufu wa Maafisa Ugani Mifugo 37 ukilinganisha na jiografia pana ya Wilaya hivyo kupelekea baadhi ya maeneo kukosa huduma stahiki ya mifugo.

MIKAKATI

Mikakati mbalimbali kuhakikisha zoezi awamu ya pili linafanyika kwa ufanisi ili kupunguza migogoro kwa kuwabaini wafugaji wavamizi. Mikakati hiyo ikiwa ni

- Kuendelea kuhamasisha na kutoa elimu kwa wafugaji na viongozi wa vijiji kuhusu umuhimu wa zoezi la utambuzi mifugo, ufugaji wa kibiashara, uvunaji mifugo na masoko ya mifugo kama mikakati wa kupunguza mifugo.

- Kuendelea na zoezi la upigaji chapa kulingana na mpango kazi ulioandaliwa **(Tizama Kiambatanisho A)**

- Kutoa vitambulisho kwa wafugaji wote halali waliosajiliwa katika rejista ya wafugaji.

- Kuimarisha ulinzi na usimamizi wa Minada ya mifugo ili Kuzuia mifugo isiyo na chapa kuuzwa mnadani, kuchinjwa machinjioni wala kukatiwa kibali cha kusafirishwa.
- Kutenga fedha ya kuendesha zoezi la chapa, katika mwaka wa fedha 2017/2018 kiasi cha Tshs. 5,863,760/- kimetengwa kutokana na vyanzo vya ndani vya mapato.
- Kuhamasisha wafugaji kuchangia asilimia 20 ya gharama za uboreshaji wa miundombinu ya mifugo na kuwashirikisha katika utekelezaji wa miradi hiyo ili Kuzuia wafugaji kuhamahama.
- Kuandaa andiko la mradi na kupeleka maombi maalumu Wizara ya Fedha (Hazina) katika bajeti ya mwaka 2017/2018 ili kuwezesha kupata fedha za Uchimbaji/Ujenzi lambo eneo la Mfilisi-Ihombwe lenye ujazo wa 209,645m^3 kwa gharama ya Tshs. 595,800,800/- (BOQ, Januari 2014).

HITIMISHO

Idara imewasilisha maombi ya mafuta na posho ofisi ya Mkurugenzi, ni matumaini yangu maombi hayo yatazingatiwa ili kuwezesha Timu ya Wataalam ngazi ya Wilaya akiwemo Mhasibu wa mapato kusimamia zoezi la chapa na ukusanyaji mapato yatokanayo na gharama ya chapa Tshs 1000/- kwa ng'ombe kwa kutumia mfumo wa kieletroniki.

Naomba kuwasilisha,

Dr. Yuda Lunodzo Mgeni
KAIMU AFISA MIFUGO NA UVUVI WILAYA
KILOSA

Kiambatanisho A: MPANGOKAZI WA AWAMU YA PILI YA ZOEZI LA CHAPA

S/N	SHUGHULI	MAHITAJI	GHARAMA	MUDA WA UTEKELEZAJI 2017									MHUSIKA
				JAN	FEBW1	FEB W2	FEBW3	FEBW4	MAR	APR	MAY	JUN	
1	Uhamasishaji na kutoa elimu kwa wafugaji juu ya umuhimu wa zoezi la chapa	Posho, Shajala, usafiri (gari na Mafuta)											DLFO
2	Kuunda timu ya Wilaya itakayosimamia zoezi la utambuzi na usajili mifugo	Wataalamu wa mifugo 6, Mhasibu mapato, Afisa Usalama											DLFO
3	Kutoa maelekezo kuhusu utambuzi na usajili kuhusu usajili wa wafugaji halali	Timu ya Wilaya, WEOs, VEOs, LFOs, Shajala											DLFO
4	Ujenzi wa mabanio 120 ya kupigia chapa mifugo	Miti, Misumari, binding wire @ 20,000	2,400,000										DLFO
5	Kupiga chapa ng'ombe	Timu ya Wilaya, WEOs, VEOs, LFOs, Posho, Shajala,	6,870,000										DLFO,
		Diesel lita 1500	3,000,000										
6	Kuingiza takwimu kwenye mfumo wa utambuzi na usajili	Mtaalamu wa mifugo, Secretary											DLFO
7	Kutengeneza na kugawa vitambulisho /kadi ya mfugaji halali aliyesajiliwa	Shajala	3,000,000										DLFO, PO
8	Ufuatiliaji na Tathmini	Usafiri, Posho, mafuta lita 300	2,075,000										DC, DED, DLFO
		Jumla Ndogo Tshs.	**17,345,000**										

Kiambatanisho B.

AWAMU YA PILI YA UPIGAJI CHAPA NG'OMBE HADI TAREHE 23/02/2017

TARAFA	KATA	IDADI YA WAFUGAJI	NG'OMBE SAJILIWA	NG'OMBE WALIOPIGWA CHAPA I	NG'OMBE WALIOPIGWA CHAPA II	JUMLA WALIOPIGWA CHAPA	ASILIMIA	MBUZI	KONDOO	PUNDA
KIDETE	Lumuma	90	1121	0		0	0	1155	172	107
	Kidete	300	3912	0		0	0	4539	786	378
Jumla ndogo		**390**	**5033**	**0**	**0**	**0**	**0**	**5694**	**958**	**485**
MIKUMI	Mikumi	256	12089	1673		1673	14	39995	2457	69
	Kisanga	193	1852	1354		1354	73	3199	845	130
	Malolo	37	111	0		0	0	1096	178	10
	Ulelingo'mbe	212	909	0		0	0	2164	95	272
	Kidodi	128	156	100		100	64	1080	76	0
	Vidunda	0	0	0		0	#DIV/0!			
	Ruaha	50	332	0		0	0	440	69	0
	Ruhembe	0	0	0		0	#DIV/0!			
Jumla ndogo		**876**	**15449**	**3127**	**0**	**3127**	**20**	**47974**	**3720**	**481**
ULAYA	Ulaya	80	3248	2800		2800	86	1128	497	31
	Zombo	101	374	94		94	25	926	16	0
	Mhenda	82	4068	378		378	9	1553	818	53
Jumla ndogo		**263**	**7690**	**3272**	**0**	**3272**	**43**	**3607**	**1331**	**84**
MASANZE	Masanze	14	3065	3065		3065	100	400	188	12
	Kilangali	121	11467	4476		4476	39	4064	2565	424
	Tindiga	34	3898	2426		2426	62	808	453	1
	Mabwerebwere	32	652	652		652	100	210	28	0
Jumla ndogo		**201**	**19082**	**10619**	**0**	**10619**	**56**	**5482**	**3234**	**437**
MAGOLE	Magole	184	2767	1462		1462	53	1533	563	5
	Dumila	462	4891	2117		2117	43	2429	518	5
	Mbigiri	53	4094	0		0	0	3615	326	5
	Kitete	375	24696	1300		1300	5	8387	5505	13
	Msowero	207	4254	1528		1528	36	1364	484	118
	Mvumi	133	4020	1019		1019	25	1547	281	106
	Mtumbatu	688	5546	5546		5546	100	7505	466	182
	Maguha	304	10386	5403		5403	52	5934	1136	9
	Magubike	359	7516	5984		5984	80	6050	1077	8
	Berega	332	5567	4480		4480	80	5347	317	14
	Mamboya	321	5619	1865		1865	33	3717	533	216
	Mabula	345	5952	0		0	0	3965	34	0
Jumla ndogo		**3763**	**85308**	**30704**	**0**	**30704**	**36**	**51393**	**11240**	**681**
KIMAMBA	Kimamba "A"	7	2463	247		247	10	871	310	0
	Kimamba "B"	22	333	333		333	100	359	36	0
	Chanzuru	54	187	63		63	34	627	0	0
	Lumbiji	78	677	0		0	0	742	269	47
	Rudewa	35	1357	1357		1357	100	349	95	18
	Madoto	266	21042	3097		3097	15	4878	1955	5
	Parakuyo	191	12892	3560	241	3801	29			
Jumla ndogo		**653**	**38951**	**8657**	**241**	**8898**	**23**	**7826**	**2665**	**70**
KILOSA MJINI	Mbumi	10	40	0		0	0	6	7	0
	Magomeni	17	3828	3828		3828	100	298	215	0
	Kasiki	24	83	0		0	0	103	16	0
	Mkwatani	137	567	0		0	0	565	50	20
Jumla ndogo		**188**	**4518**	**3828**	**0**	**3828**	**85**	**972**	**288**	**20**
JUMLA KUU		**6334**	**176031**	**60207**	**241**	**60448**	**34**	**122948**	**23436**	**2258**